


Mkulima akilima shamba kwa kutumia trekta aina ya Power Tiller. Ukosefu wa elimu kwa wakulima unatajwa kuwa moja ya sababu ya wakulima wengi kutokuwa na tija katika kilimo. **Picha ya Maktaba**

# Elimu; kikwazo kwa maendeleo ya wakulima

**Ubunifu ni ufunguo wa ushindani katika soko lolote. Teknolojia mpya katika uzalishaji ndiyo msingi wa tija katika maendeleo ya kiuchumi duniani.**

Veneranda Sumila, Mwananchi

Wakulima na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo nchini wana nafasi kubwa ya kufanyabiashara katika soko la pamoja la Afrika Mashariki kama kutakuwepo na mabadiliko katika sera za biashara zilizopo sasa za mazao ya kilimo kutoka Tanzania.

Ingawa serikali imesema wazi kwamba inatoa kipaumbele kwa sekta ya kilimo, wataalamu wanasema kwamba kukosekana kwa utaratibu wa kuoanisha sera na kanuni za kisera zenye lengo la kupunguza urasimu na kusukuma utekelezaji wa sheria zilizopo, unanyima fursa wakulima na wafanyabiashara wa mazao ya kilimo.

"Ni ngumu sana kwa Tanzania kushindana katika soko la pamoja na Afrika Mashariki kwa sababu kama taifa halijajiandaa kufanya biashara na wengine na badala yake inajishughulisha na mambo yake ya ndani," alisema Mkurugenzi Mtendaji wa Shirikisho la Wafanyabiashara wanaosafirisha bidhaa nje, Mtemi Naluyaga.

Kwa mujibu wa Naluyaga Tanzania ikitumia kwa makini eneo lake la ardhi linalozalisha bidhaa za kilimo itakuwa na uwezo wa kuongeza biashara ya bidhaa zake za kilimo kwa mataifa jirani.

"Lakini kwa sasa kuna vikwazo vingi vinavyowanyima fursa wakulima kuzalisha zaidi, kwani kwa mtu kuweza kusafirisha bidhaa zake anatakiwa kuwa na ruksa ambayo si rahisi kuipata," alisema Naluyaga.

Kwa mujibu wa mtendaji huyo wakati wazawa wanakataliwa kupata vibali vya kusafirisha bidhaa kupeleka nje, wageni wengi hasa Wakenya wanaingia nchini na kununua bidhaa za Tanzania kwa bei ya kutupa na kuvuka mpaka bila kutambuliwa.

Alisema mwezi uliopita pekee zaidi ya tani 50,000 za mahindi katika soko la kimataifa la Kibaigwa zilinunuliwa na Wakenya na kusafirishwa lakini hakuna takwimu zinazoonyesha kwamba kiasi hicho cha nafaka kimevuka mpaka.

"Hili ni jambo linaloudhi sana hasa ikijulikana dhahiri kwamba hakuna Mtanzania anayeweza kununua nafaka kutoka Kenya," alisema.

Hata hivyo utafiti uliofanywa kwa msaada wa BEST AC kuhusu matumizi ya soko hilo kwa Watanzania, umebainisha kwamba kikwazo kikubwa ni elimu.

"Kundi kubwa lililopo katika mnyororo wa thamani katika kilimo (AVC) ni wale ambao hawajasoma! Hii inamaanisha kwamba ni vigumu sana kufanya kilimo kuwa cha ushindani," inasema ripoti ya utafiti huo.

Tatizo hilo la elimu ndilo hasa linawakwaza hata watu wa taasisi za fedha wanapoangalia uwezekano wa kukopesha wakulima au kutoa mikopo katika sekta ya kilimo.

Tanzania kwa sasa ipo katika mgogoro mkubwa kuhusiana na ubora wa elimu yake ya msingi na ukiangalia ukweli kwamba wengi wa watu wanaoshiriki katika mfumo huo wa uzalishaji katika kilimo wakiwamo wakulima wenyewe, wafanyabiashara na wasafirishaji ni wale wa elimu ya msingi.

Na inajulikana wazi kwamba wengi wa wanafunzi wanaomaliza darasa la saba wanamaliza shule bila kujua kusoma wala kuandika.

"Hali ya elimu ya shule ya msingi Tanzania ni mbaya kiasi ya kwamba nivigumu sana kuwaingiza vijana hawa katika kilimo cha kisasa ambacho kina teknolojia iliyoboreshwa," inasema ripoti hiyo.

Kwa mujibu wa wataalamu ni vigumu sana kuongeza thamani ya bidhaa za shambani kutokana na watu wanaohusika na kilimo kutokuwa na elimu ya kutosha. Mapitio ya sekta ya kilimo ya mwaka 2009/10 yanaonesha kwamba wazalishaji wadogo katika sekta hiyo hawajawahi kupatiwa mafunzo juu ya usindikaji wa bidhaa zao za kilimo kutokana na kutokuwapo kwa wataalamu wa kutoa mafunzo ya usindikaji wa bidhaa za kilimo.

Aidha ripoti ya utafiti imeonyesha kwamba miradi mingi ya usindikaji haitekelezwi kwa muda unaotakiwa kutokana na kukosekana kwa wataalamu wa kuelekeza utekelezaji wa miradi hiyo.

"Chama cha Wenye Viwanda Biashara na Kilimo, (TCCIA) ni vyema kikajenga uwezo kwa wafanyakazi wake katika wilaya na wale wa halmashauri ili kuwezesha biashara kwa kuzingatia mazingira ya soko la pamoja la Afrika Mashariki," imesema ripoti.

Kwa mujibu wa ripoti, TCCIA kwa kushirikiana na Shirika la Viwango nchini (TBS) na wakala wengine wanaosimamia sheria na kanuni kwenye bidhaa za kilimo wanawajibika kuwaelimisha wananchi kuhusu sera, kanuni na viwango kuhusu bidhaa za sekta ya kilimo ili kuzipa hadhi na ushindani katika soko la pamoja la Afrika Mashariki.

"Kwa mujibu wa matokeo ya utafiti huo, wafanyakazi wa sekta ya umma na wa serikali hawajajihamasisha kutambua umuhimu wa biashara na mchango wake katika ukuaji wa uchumi na pato la taifa.

Kutokana na hilo ni dhahiri mafunzo yanatakiwa ili kuwapa ufahamu na kutambua namna ya kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wa kilimo," inasema ripoti ya utafiti iliyofadhiliwa na BEST AC.

Hata hivyo Bw Naluyaga ameitaka Serikali kutengeneza sera ya mauzo ya bidhaa za kilimo nje ili kushawishi biashara zaidi ya bidhaa za kilimo kwenda nje.

"Nchi yetu haina sera ya usafirishaji bidhaa kwenda nje, na badala yake inategemea sera ya biashara, kutengenezwa kwa sera ya uuzaji bidhaa nje kutachochea biashara ya bidhaa za kilimo za Tanzania."

## HABARI ZAIDI

**Miundombinu ya umma Tanzania ni dhaifu. Utegemezi mkubwa wa barabara umesababisha biashara ya kilimo kuwa ngumu na hali hasa barabara hizo zinapoharibika wakati wa mvua.**

**Kutokana na ubovu wa barabara wasafirishaji wamekuwa wakilazimika kutumia magari ya ekseli moja kubeba mizigo. Magari haya kwa bahati mbaya yanalazimika kujazwa mizigo na hivyo kuvutia wanausalama katika vizuizi vya barabarani kutaka rushwa.**

BEST-AC
Tuboreshe mazingira ya biashara
Doing business, let's make it easy
UKURASA HUU UNADHAMINIWA NA BEST-AC NA MWANANCHI